

Tangazo la Serikali Na. 116 la tarehe 25/04/2014

SHERIA ZA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA, 1982

(SURA YA 290)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya Kifungu cha 7(1)(e) na 16(1)

**SHERIA NDOGO ZA USHURU WA MADINI YA UJENZI ZA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA, 2014**

SEHEMU YA I

MASHARTI YA MWANZO

- | | |
|-----------------------------------|--|
| Jina na tarehe ya kuanza kutumika | 1. Sheria ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za Ushuru wa Madini ya Ujenzi za Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, 2014 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali. |
| Matumizi | 2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya halmashauri ya Wilaya ya Muheza |
| Tafsiri
Sura ya 290 | 3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo:-
“Sheria” maana yake ni Sheria za Fedha za Serikali za Mitaa;
“Mwenyekiti”
(a) Kwa madhumuni ya Halmashauri maana yake ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya. |

(b) Kwa madhumuni ya Kamati, Bodi au Kamati Ndogo maana yake ni Mwenyekiti wa Kamati, Bodi au Kamati Ndogo.

“Ada” maana yake ni malipo ambayo kila mmiliki wa machimbo ya madini ya ujenzi anatakiwa kulipa;

“Ushuru” maana yake ni malipo ambayo kila mnunuzi wa madini ya ujenzi atatakiwa kulipa;

“Kibali” maana yake ni idhini inayotolewa na Halmashauri kuruhusu uchimbaji madini ya ujenzi;

“Madini ya ujenzi” maana yake ni mawe, changarawe, mchanga, udongo wa mfinyanzi, kifusi, kokoto au chokaa, au chochote kinachopatikana na kuchimbwa katika eneo la mamlaka ya Halmashauri;

“Maeneo yasiyoruhusiwa” maana yake ni mito, madaraja, barabara, mashamba ya watu, maeneo ya miji na shule;

“Wakala” maana yake ni mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni au taasisi iliyokasimiwa jukumu la ukusanyaji wa ushuru wa madini kwa niaba ya Halmashauri;

“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Muheza.

“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri au mtu yeyote aliyeteuliwa kufanya kazi za Mkurugenzi.

“Waziri” maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa;

“Afisa Muidhiniwa” maana yake ni Afisa yeyote ambaye anasimamia utekelezaji wa sheria ndogo hizi;

SEHEMU YA II

UTARATIBU WA KUKUSANYA USHURU

- Ada ya umiliki wa machimbo 4
- (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayetaka kuanzisha machimbo ya madini ya ujenzi kutoa taarifa kwa Mkurugenzi ili eneo hilo likaguliwe kuona kama linakidhi matakwa ya sheria za mipango Miji na Hifadhi ya Mazingira;
 - (2) Ada ya kuanzisha madini itakuwa ni shilingi Laki moja;
 - (3) Halmashauri inaweza kukataa au kukubali eneo lolote kuwa machimbo ya madini ya ujenzi;
 - (4) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa machimbo ya madini ya ujenzi kuhakikisha kwamba analipa ada ya shilingi laki moja [100,000/=] kwa Halmashauri ikiwa ni ada ya umiliki kwa mwaka;
 - (5) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kufunga machimbo yoyote yaliyofunguliwa bila ya kufuata utaratibu au yanayoendeshwa bila kuzingatia matakwa ya sheria ndogo hizi;
- Ushuru wa madini ya ujenzi 5
- (1) Halmashauri iatatoza ushuru wa madini ya ujenzi kutoka kwa mtu yeyote atakayesafirisha madini ya ujenzi kutoka eneo madini ya ujenzi yanakochimbwa kwenda maeneo mengine kwa kila tripu kwa viwango vilivyoanishwa katika sheria ndogo hizi;

- (2) Ushuru huo utatozwa katika eneo la machimbo au eneo lolote la mamlaka ya Halmashauri endapo madini husika yatakuwa hayajalipiwa ushurui katika eneo la machimbo;
- (3) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kumzuia dereva yeyote wa gari lolote linalosafirisha madini ya ujenzi bila kufuata utaratibu uliowekwa katika sheria ndogo hizi;
- Malipo ya ushuru 6 (1) Ushuru au ada itakayotozwa chini ya sheria ndogo hizi italipwa kwa halmashauri ama wakala aliyeteuliwa na halmashauri kwa mujibu wa sheria;
- (2) Halmashauri au wakala wanawajibika kutoa stakabadhi halali kwa malipo yaliyofanywa na mlipa ushuru au mlipa ada aliyehusika;
- Muda wa kufunga machimbo 7 (1) Maeneo yote ya machimbo ya madini ya ujenzi yatafunguliwa saa kumi na mbili alfajiri na kufungwa saa kumi na mbili jioni'
- (2) Si ruhusa kwa mtu yoyote kufanya shughuli zozote kabla au baada ya muda uliotajwa katika sheria ndogo 7(1) hapo juu.
- Vituo ukaguzi vya 8 (1) Halmashauri itaanzisha kituo cha ukaguzi wa magari yanayobeba madini ya ujenzi katika barabara ziingiazo na kutoka katika eneo la Halmashauri;
- (2) Kila dereva atawajibika kusimama katika kituo cha ukaguzi wa madini ya ujenzi na kuonyesha stakabadhi ya malipo ya malipo ya ushuru wa madini ya ujenzi na endapo mhusika atakuwa hana stakabadhi ya malipo atawajibika kulipa kwa viwango vilivyoainishwa katika jedwali la sheria ndogo hizi.

Taratibu za uchimbaji	9	(1)	Itakuwa ni marufuku kwa mtu yoyote kuchimba au kuhamisha madini ya ujenzi kutoka katika eneo la Halmashauri bila kibali cha Halmashauri.
		(2)	Mtu yeyote anayejishughulisha na uchimbaji wa madini ya ujenzi atatakiwa kuzingatia sheria za mazingira na endapo kuna ukiukwaji wa Sheria za mazingira, halmashauri inaweza kusimamisha shughuli za uchimbaji unaofanywa iwapo itabainika kwamba kufanya hivyo ni muhimu ili kuokoa mazingira.
Marufuku kuchimba	10	(1)	Itakuwa ni marufuku kwa mtu yoyote: <ul style="list-style-type: none"> (a) Kuchimba madini ya ujenzi katika maeneo yasiyoruhusiwa; (b) Kuchimba madini ya ujenzi kwenye maeneo ya mito au kando ya mito na vyanzo vya maji; (c) Kuchimba madini ya ujenzi ndani ya mita thelathini kutoka kwenye ukingo wa barabara au uwanja wa ndege au chanzo cha maji.
Halmashauri kutenga eneo	11	(1)	Halmashauri itatenga na kutangaza maeneo yanayoruhusiwa kuchimba madini.
		(2)	Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba madini ya ujenzi katika maeneo ambayo hayajaruhusiwa na Halmashauri;
Uwezo wa afisa muidhiniwa	12	(1)	Afisa Muidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika eneo lolote wakati wa saa za kazi kukagua utekelezaji wa sheria ndogo hizi na mtu yeyote atakaye.
		(2)	Afisa Muidhiniwa anaweza kuzuia gari lolote ambalo limebeba madini ya ujenzi ambayo hayajalipiwa ushuru chini ya sheria ndogo hizi.
Makosa	13		Mtu yeyote atakayevunja au kushindwa kutekeleza sharti lolote chini ya sheria ndogo hizi atakuwa ametenda kosa chini ya sheria ndogo hizi na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi 300,000/= [shilingi laki tatu] au kutumikia kifungo cha miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa ujumla faini na kifungo.

- Msamaha 14 (1) Halmashauri inaweza kuamuru madini ya ujenzi kuchimbwa au kusafirishwa bila kulipia ushuru iwapo msafirishaji ameomba kibali na halmashauri imeridhia kutokana na sababu za msingi alizozitoa mhusika;
- (2) Sababu zinazoweza kutolewa zitajumuisha:
- (a) Madini husika yatatumika kutekeleza miradi ya kijamii;
 - (b) Madini yatatumika kwa manufaa ya taasisi za kidini na kiserikali;
 - (c) Sababu nyingine zinazoweza kukubalika kulingana na hali iliyojitokeza.
- Kufilisha kosa 15. Mkurugenzi anaweza kufilisha kosa kwa kumtoa mtua au taasisi faini isiyozidi shilingi 100,000/= [shilingi laki moja] endapo mhusika atakiri kwa maandishi kutenda kosa kwa kujaza fomu maalum iliyoambatanishwa kwenye jedwali la sheria ndogo hizi na kukubali kulipa faini na kiasi cha ada au ushuru anachodaiwa.

JEDWALI LA KWANZA

Aina ya gari	Kiwango cha ushuru
Gari Tani 1 – 3	shilingi 3,000/= kwa tripu
Gari tani 4-7	shilingi 4,000/= kwa tripu
Gari tani 8-12	shilingi 5,000/= kwa tripu
Gari tani 13 na kuendelea	shilingi 7,000/= kwa tripu

JEDWALI LA PILI

**SHERIA NDOGO ZA USHURU WA MADINI YA UJENZI
ZA HALMASHAURI YA WILAYA MUHEZA, 2014**

Mimi nakiri mbele ya Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya wilaya ya Muheza kwamba, mnamo tarehe mwezi mwaka nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kifungu cha Cha sheria ndogo za madini ya ujenzi za Halmashauri ya Wilaya ya Muheza za mwaka 2014. Nipo tayari kulipa cha ushuru/ada ninayodaiwa pamoja na faini ikiwa Mkurugenzi Mtendaji atatekeleza mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 7 cha sheria ndogo hizi.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiyari yangu na kwa kadri ya ufahamu wangu.

Tarehe

Saini:.....

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ilibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuata azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 31 mwezi wa 10 Mwaka 2012 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:

.....
Ibrahim Matovu
MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA
MUHEZA

.....
Amir Abdulrahman Kiroboto
MWENYEKITI WA HALMASHAURI YA WILAYA
MUHEZA

Nakubali

.....
Mhe. MIZENGO PETER KAYANZA PINDA
WAZIRI MKUU

DODOMA.

Tarehe.....